


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA NGORONGORO.
(Barua zote zitumwe kwa Mkuu wa Shule)**



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. SSS/S2560/ADMIN/VOL.1/109

Tarehe

NDUGU
K.K
MWALIMU MKUU
SHULE YA MSINGI,.....

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA 2021.

1.0 UTANGULIZI

Ninayo furaha kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga Kidato cha kwanza katika Shule ya Sekondari **SAMUNGE**. Hongera sana .Unatakiwa kuitumia nafasi hii vizuri kwa kusoma kwa bidii na kufanya kazi zote kwa kujituma kwa wakati wote uwapo hapa Shulenii kwa manufaa yako na Taifa kwa ujumla ikiwa ni pamoja na kufuata kanuni,Sheria na taratibu za Shule.

2.0 KUFUNGUA SHULE.

Shule itafunguliwa tarehe **11-01-2021** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **15-01-2021**. Ni vema uwepo siku hiyo.Unatakiwa kuripoti Shulenii saa **3:00 asubuhi** bila kukosa. Shule ipo wilaya ya Ngorongoro, Tarafa ya Sale,Kata ya **SAMUNGE**-(Jina maarufu "**KWA BABU WA SAMUNGE**"),Kijiji cha **SAMUNGE**.Yapo mabasi ya kutosha Arusha hadi Samunge,Yapo pia mabasi kutoka karatu,Ngorongoro hadi Loliondo na kutoka loliondo/Wasso hadi Samunge. Unapokuja kuripoti Shulenii teremka Samunge madukani utakuta kibao kinacho elekeza mahali Shule ilipo.

Shule ipo upande wa Magharibi umbali wa mita **800** kutoka barabara kuu ya kutoka Loliondo-Arusha kuititia Digodigo au Arusha Digodigo – Loliondo.

3.0 VIFAA VYA KUJA NAVYO SHULENI

- i. Baadhi ya vifaa vyta darasani unavyotakiwa kuja navyo
 - ❖ Daftari 15 (Counter book Quire 3) na **kalamu** za kutosha
 - ❖ Madaftari madogo 6 kwa ajili ya mazoezi
 - ❖ Rula 1
 - ❖ Mathematical set 1
 - ❖ Dictionary Oxford – English to English
 - ❖ **Vitabu binafsi** vyta rejea vyta masomo yanayofundishwa Sekondari vyta kidato husika.
 - ❖ **Begi la kubebea** madaftari na vitabu (Mifukoya plasic ni marufuku kuonekana nayo hapa Shulenii)



Edit with WPS Office

- ❖ File kwa matumizi binafsi kwa ajili ya kutunza kumbukumbu za masomo hasa mitihani (Past paper)
- ❖ Unatakiwa kuja na **Rim paper** (Karatasi nyeupe) kwa matumizi binafsi hasa kipindi cha majaribio ya wiki na mwezi.

ii. Vifaa na mahitaji mengine ya **Mwanafunzi**

- ❖ Vyombo vya kulia chakula (Sahani,Kikombe,Bakuli na kijiko –Sahani za bat (Aluminium) au mifupa
- ❖ Taulo ya kuogea/ Kanga pea mbili kwa wasichana
- ❖ Ndala za kuogea
- ❖ Shuka mbili au zaidi za rangi ya light blue.
- ❖ Toilet paper za kutosha kwa matumizi binafsi
- ❖ Uje na sanduku la chuma (trunk) lililo imara na kofuli imara.
- ❖ Uje na ndoo ya maji ya lita 10 kwa matumizi binafsi
- ❖ **MUHIMU SANA.**Uje na Godoro la sponchi la futi $2\frac{1}{2}$ au $3\frac{1}{2}$ kwa 6 lenye foronya na aina ya "TAN FORM". Aina nyingine ya magodoro yamebainika kusinyaa mapema sana baada kutumiwa.
- ❖ Dawa ya meno,Mswaki,Kiwi,Chandarua,Mafuta ya kujipaka,Sabuni miche 3 au Zaidi

iii. Vifaa vya usafi

- ❖ Mvulana aje na Jembe lenye mpini na hard broom ngumu kwa ajili ya usafi ya maeneo yao ya usafi watakayopangiwa
- ❖ Msichana aje na Jembe lenye mpini na Fagio za chelea kwa ajili usafi wa maeneo ya usafi atakayopangiwa

5.0 SARE ZA SHULE

(i).SARE YA WAVULANA

- ❖ Suruali – Kijani kibichi - pea mbili gred One(Sampuli imeambatanishwa)
- ❖ Shati jeupe la mikono mifupi, Pea mbili aina ya Tomato
- ❖ Sweta – Rangi ya kijani kibichi pea mbili
- ❖ Soksi Nyeupe Pea tatu au zaidi
- ❖ Viatu vyeusi vya Ngozi vya kamba visivyo na kisigino kirefu
- ❖ Tai- Tai iwe ya kijani kibichi inayofanana na Suruali.
- ❖ Mkanda wa ngozi mweusi wa suruali usio na bakoli kubwa.
- ❖ Tisheti ya Njano yenye nembo ya Shule pea moja au zaidi (Tisheti zinapatikana ma jirani na Shule)

(ii).SARE YA WASICHANA

- ❖ Sketi – Kijani kibichi - pea mbili gred One(Sampuli imeambatanishwa)
- ❖ Shati jeupe la mikono mifupi, Pea mbili aina ya Tomato
- ❖ Sweta – Rangi ya kijani kibichi pea mbili
- ❖ Soksi Nyeupe Pea tatu au zaidi
- ❖ Viatu vyeusi vya Ngozi vya kamba visivyo na kisigino kirefu
- ❖ Tai- Tai iwe ya kijani kibichi inayofanana na Suruali.
- ❖ Mkanda wa ngozi mweusi wa suruali usio na bakoli kubwa.
- ❖ Tisheti ya Njano yenye nembo ya Shule pea moja au zaidi (Tisheti zinapatikana ma jirani na Shule)

(iii). **SARE ZA INJE YA DARASA- SHAMBA DRESS**

- Rangi ya light bluu suruali na shati mikono mifupi.
- Rangi ya lightbluu suruali na blauz ya mikono mifupi kwa wasichana

(iii). **SARE ZA MICHEZO**

- Track suit rangi Nyekundu yenye mistari nyeupe pembedni na iwe ya mtelezo sio nzito. "**MUHIMU**" isiwe inabana mwili na miguuni (Mnyonyo) kwa wavulana na wasichana

- Raba za michezo na soksi za michezo
- Tisheti ya michezo rangi nyekundu- isiwe yenyenye nembo ya timu ye yeyote kwa wavulana na wasichana
- Bukta nyekundu kwa wavulana na wasichana

NB- Vitambaa vya sare, shamba dress na trak suit zinapatikana maduka yaliyopo jirani na Shule.

5.0 MAMBO YA KUZINGATIA/KUFAHAMU

- Mwanafunzi hataruhusiwa kumiliki simu ya mkononi, ni kosa kubwa ukikutwa nayo unafukuzwa Shule mara moja.
- Siku ya kuripoti mwanafunzi anatakiwa kuva sare ya kushindia (Shamba dress)
- Shule haina utaratibu/uwezo wa kutoa chakula maalum(Special diet) kwa wanafunzi wenyewe matatizo ya kiafya
- Hairuhusiwi kuonekana nje ya eneo la mipaka ya Shule isipokuwa kwa kibali maalumu kutoka ofisi ya malezi
- Hairuhusiwi kuwa na vitu vingine vya thamani mbali na unavyoolekezwa kwenye fomu hii(Fedha za matumizi ziabidhiwe ofisi ya malezi)

6.0 MUHIMU

- Unatakiwa upimwe kwenye Hospitali ya Serkali kuthibitisha kama afya yako inafaa kwa masomo.Tumia fomu iliyombatanishwa.
- Ili kuepuka usumbufu wakati wa kupolewa siku ya kuripoti unatakiwa kutekeleza maagizo yote yaliyotolewa hapo juu.
- Unaporipoti Shuleni utakabidhiwa Sheria za Shule ujisome, uzielewe na uzifuate.
- Unatakiwa kurejesha fomu ya Hospitali siku unaporipoti Shuleni.

FOMU HII IMEJADILIWA NA KAMATI YA UONGOZI WA SHULE (SMT) NA KUIDHINISHWA NA BODI YA SHULE.

KARIBU SHULE YA SEKONDARI SAMUNGE

OTTO PIUS SANAYA

MKUU WA SHULE-0786 69 48 11 / 0764 17 92 80

Nakala

1. Mthibiti ubora wa Shule kanda

Kaskazini Magharibi

S.L.P

ARUSHA

2. Katibu Tawala Mkao wa Arusha

S.L.P,

Arusha

3. Mkurugenzi Mtandaji(W)

Wilaya ya Ngorongoro

S.L.P 1,

LOLIONDO

4. Afisa Elimu Wilaya (Sekondari).



Edit with WPS Office

Wilaya ya Ngorongoro
S.L.P 1,
LOLIONDO

FOMU 4

SAMUNGE SECONDARY SCHOOL, BOX 47, LOLIONDO

MEDICAL EXAMINATION REPORT FOR STUDENTS.

To be completed by a government, Medical Officer.

Pupil's full name

Blood count (red and white)

Stool examination

Urinalysis

T.D Test

Eye test

Ears

Chest

Spleen

Abdomen

Additional information e.g. Physical defects or impairment infection chronic or Family shape etc.

TO BE COMPLETED BY GOVERNMENT MEDICAL OFFICER.

I certify that the above – mentioned pupil is fit to pursue his/her further studies

Signature

Designation

Station

Date



Edit with WPS Office



Edit with WPS Office